



Kasarani Campus  
Off Thika Road  
P. O. Box 49274, 00101  
NAIROBI  
Westlands Campus  
Pamstech House  
Woodvale Grove  
Tel. 4442212  
Fax: 4444175

**KIRIRI WOMEN'S UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY**  
**UNIVERSITY EXAMINATION, 2023/2024 ACADEMIC YEAR**  
**THIRD YEAR, FIRST SEMESTER EXAMINATION**  
**FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION(ARTS)**  
**KSW 2302:RESEARCH METHODS IN LANGUAGE & LITERATURE**

Date: 7<sup>th</sup> December 2023

Time: 11:30am-1.30pm

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES:**

**ANSWER QUESTION ONE (COMPULSORY) AND ANY OTHER TWO QUESTIONS**

**QUESTION ONE (30 MARKS)**

- a) "Umuhimu wa mandhari katika kustawisha maudhui katika riwaya ya *Chozi la Heri*." Ukirejelea mada hii:
- Buni malengo **manne** mahususi. (alama 4)
  - Eleza namna utakavyoteua sampuli katika utafiti huu. (alama 4)
  - Fafanua namna utakavyokusanya na kuchanganua data katika utafiti huu. (alama 6)
- b) Eleza kwa ufupi sababu zinazoleta haja ya kufanya utafiti. (alama 6)
- c) Kabla ya kila utafiti wa nyanjani kufanyika, maandalizi mwafaka hufaa kufanywa. Jadili matayarisho yanayofaa kufanywa kabla ya mtafiti kwenda nyanjani. (alama 6)
- d) Fafanua dhana zifuatazo na namna zinavyotumika katika taaluma ya utafiti katika Kiswahili:
- Utafiti. (alama 2)
  - Pendekezo la utafiti. (alama 2)

**QUESTION TWO (20 MARKS)**

- Pambanua umuhimu wa nadharia katika utafiti wa Kiswahili. (alama 6)
- Jadili dhima ya mwauo wa maandishi katika pendekezo la utafiti. (alama 6)
- Fafanua manufaa ya vifaa vifuatavyo vya utafiti kwa mtafiti:
  - Tansifu. (alama 4)
  - Faharasa. (alama 4)

**QUESTION THREE (20 MARKS)**

- Kwa kutoa mifano, fafanua tofauti kati ya dhana zifuatazo:
  - Nadharia na nadharia tete. (alama 2)
  - Nakala dhanishi na pendekezo la utafiti. (alama 2)
- Ni nini maana ya sampuli? (alama 2)
- Bainisha aina zozote **tatu** za sampuli. (alama 6)
- Unafanya utafiti kuhusu athari za mihadarati katika katika masomo ya wanafunzi katika chuo kikuu unakosomea.
  - Ikiwa unatumia mbinu ya mahojiano, taja makundi **matatu** ya watu utakao wahoji katika utafiti huu. (alama 3)

- ii) Jadili udhaifu wa mbinu ya mahojiano katika kuibua data zitakohitajika kufanikisha utafiti huu. (alama 3)
- iii) Fafanua changamoto za kutumia hojaji wazi katika utafiti huu. (alama 2)

**QUESTION FOUR (20 MARKS)**

- a) Bainisha na kuyaeleza maadili yoyote **sita** yanayohitajika kuzingatiwa katika utafiti. (alama 6)
- b) Jadili masuala **mawili** yanayoweza kufanya mada ya utafiti kutofikia viwango vifaavyo katika utafiti. (alama 4)
- c) Fafanua changamoto zinazoweza kumkumba mtafiti nyanjani. (alama 6)
- d) Eleza changamoto za utafiti wa maktabani. (alama 4)

**QUESTION FIVE (20 MARKS)**

- a) Sehemu ya marejeleo katika pendekezo la utafiti inastahili kudhihirisha sifa fulani. Jadili sifa zozote **sita**. (alama 6)
- b) Fafanua utafiti wa kimaelezo na utafiti wa kitakwimu. Kwa kila aina ya utafiti, toa mfano **mmoja mmoja** wa utafiti unaoweza kufanywa ukitumia aina husika ya utafiti. (alama 4)
- c) Eleza masuala unayostahili kuzingatia unapofanya uhakiki wa maandishi katika utafiti. (alama 4)
- d) Fafanua dhana zifuatazo za utafiti.
  - i) Mbinu za utafiti. (alama 2)
  - ii) Vifaa vya utafiti. (alama 2)
  - iii) Upeo wa utafiti. (alama 2)